Daudi

Mvulana mchungaji

TRUEWAY KIDS.COM

Utangulizi

Somo la Biblia la wiki hii linatoka katika 1 Samweli 16:1-13, ambapo Samweli anampaka mafuta Daudi, Mvulana mdogo mchungaji, kuwa mfalme anayefuata wa Israeli.

Baadhi ya mambo muhimu tutakayochunguza ni:

- Tunahitaji kumaliza vizuri.
- Mungu anaangalia mioyo ya watu na sio muonekano wao wa nje.
- Mungu hutumia vitu vidogo kututayarisha kwa mambo makubwa.
- Tunahitaaji kuwa na subira na kusubiri ahadi za Mungu.

Mwongozo wa somo

Anza somo la wiki hii kwa kurejea somo kuhusu Mfalme Sauli. Eleza jinsi watu walivyotaka mfalme awe kama watu wengine. Walifurahishwa na Mfalme Sauli kwa sababu alionekana kuwa Mfalme mzuri. Alikuwa mrefu, mzuri na mwenye nguvu. Alionekana kama Mfalme. Eleza kwamba alianza vizuri, lakini muda mfupi baadaye, mambo yalikwenda vibaya.

Tumia fursa hii kuzungumza na watoto wako kuhusu kumaliza vizuri. Elezea kwamba sio tu juu ya kuanza kitu vizuri. Fikiria baadhi ya mifano: mfano labda wanaweza kutayarisha vitu vyao vya kuchezea vizuri, lakini wakachoka na kuviacha katika kuvurugika. Labda wanasikiliza vizuri maagizo Fulani na baadaye wanaanza kufanya mambo yao wenyewe.

Shirikisha jinsi Mfalme Sauli alivyoanza kufanya mambo yake mwenyewe na hivyo Mungu akamwambia Samweli ni wakati wa Kumpaka mafuta Mfalme mpya wa Israeli.

Soma kifungu cha jinsi Samweli alivyoenda nyumbani kwa Yese. Eleza jinsi Yese alivyowaonyesha wana wake wote na karibu kumsahau Daudi kwa sababu alikuwa shambani na kondoo. Waulize watoto wako kama wanafikiri mvulana mdogo anayechunga kondoo angeweza kuwa Mfalme mzuri?

Kata baadhi ya picha za watu kutoka kwenye gazeti au mtandaoni. Acha mtoto wako achague watu tofauti kwa shuguli tofauti. Kwa mfano, mtu wa kuimba, mtu wa kubeba kitu kizito, mtu wa kusaidia, mgonjwa na kadhalika. Eleza jinsi mara nyingi tunavyowahukumu watu kulingana na jinsi wanavyoonekana, lakini Mungu anajali sana kile tunachopenda kwa ndani.

Wakumbushe watoto wako kwamba wao si wadogo sana kwa matumizi ya Mungu.

Eleza jinsi Daudi alivyochunga vizuri kondoo wa baba yake shambani. Fikiria juu ya vitu ambavyo kondoo wanahitaji: Chakula, maji, ulinzi, makao, na kadhalika. Unaweza kusafiri kwenye shamba la karibu kutembela/kutazama kondoo pamoja na watoto wako.

Shirikisha jinsi Mungu alivyoona kwamba Daudi alikuwa na moyo mzuri na kweli alichunga kondoo. Mungu alijua kwamba ikiwa angechunga kondoo vizuri angewatunza pia watu wake vizuri. Wakumbushe watoto wako jinsi ilivyo muhimu kufanya mambo madogo na makubwa vizuri. Soma Wakolosai 3:23-24 “Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana.”

Zungumza na watoto wako kuhusu kuwa na subira. Wakumbushe kwamba unapoahidi kitu, utatimiza ahadi yako, lakini wakati mwingine lazima wasubiri. Kwa mfano, nitakupeleka kwenye bustani mchana huu. eleza kwamba ingawa Daudi alipakwa mafuta na Samweli kuwa Mfalme, ilimbidi kungoja muda mrefu kabla ya kuwa mfalme. Ni lazima tungojee ahadi za Mungu, lakini Mungu hutimiza ahadi zake daima.

© 2023 truewaykids.com

Samweli alipomwona Daudi, akajua ni yule ambaye Mungu amemchagua.

Mungu aliuona moyo wa Daudi.

Samweli alichukua mafuta na kumpaka Daudi.

Daudi hakuwa mfalme mara moja, lakini alijua Mungu alikuwa na mpango maalum kwa ajili yake.

Mfalme mpya

Muda mfupi baada ya Sauli kuwa mfalme, alianza kuwa na kiburi.

Aliacha kumtii Mungu na kuanza kufanya mambo yake mwenyewe.

Sauli alifikiri angeweza kufanya anachotaka mradi tu aombe msamaha baada ya kutenda.

Samweli alihuzunika.

Mungu alimwambia Samweli kuwa ni wakati wa kutafuta mfalme mpya.

Mungu alimwambia Samweli aende Bethlehemu kwa na kwa mtu/mwanamume aitwae Yese.

Samweli alimwomba Yese awalete watoto wake ili ampake mafuta mmoja wao.

Mtoto/mwana wa kwanza wa Yese alikuwa mrefu, mwenye nguvu na mzuri. Samweli alifikiri anaonekana kama mfalme. Lakini Mungu alisema, “Hapana.”

Akawaleta wanawe wengine, lakini Mungu akaendelea kusema, “La”, si huyu.”

Samweli akamuuliza Yese kama alikuwa na wana wengine?

Yese akasema, “Ni mdogo tu, lakini yuko nje shambani akichunga kondoo.”

Daudi alikuwa mvulana/ kijana mdogo tu. Hakuna aliyefikiri angeweza kuwa mfalme.

Samweli akamwambia Yese amlete Daudi kwake.

Michezo na kazi

Huwezi kuhukumu kitabu kwa jalada lake

Mpeleke mtoto wako kwenye maktaba ya karibu nawe. Waambie wachague baadhi ya vitabu ambavyo wanadhani vinapendeza kusoma.

Elezea kifungu “usihukumu kitabu kwa jalada lake.” Eleza jinsi tunavyohitaji kuangalia ndani na nje.

Ningechagua…

Weka baadhi ya vitu vya nyumbani juu ya meza.

Eleza tatizo ulilonalo. Kwa mfano, “ninahitaji kitu cha kunywa nacho.”

Mtoto lazima achukue bidhaa bora zaidi. Ikiwa ana umri mkubwa, unaweza pia kuwauliza kwa nini walichagua kitu hicho.

Kondoo wa puto

Waulize watoto wako kufikiria kwamba puto ni kondoo. Unaweza kuchora nyuso katika puto zingine.

Wafanye wachunge wakiwaweka mahali pamoja.

Wakati wanapokuwa hawaangalii, unaweza kuficha moja ya kondoo. Wakati wowote watakapompata, lazima wamrudishe kwa kondoo wengine.



© 2023 truewaykids.com

Watu hawa wana urefu gani?



© 2023 truewaykids.com

Fuatilia na upake rangi



Naweza kuhesabu ☐ mioyo

© 2023 truewaykids.com

Kata nyuma ya kila kondoo na gundisha ili kufanana



© 2023 truewaykids.com

Linganisha watu na maneno

fidhuli

haraka

nguvu

dhaifu

furaha

© 2023 truewaykids.com

Ufundi wa kondoo wa sufi

Utahitaji:

nakala ya ukurasa ya kupaka rangi (kondoo)
penseli za rangi/kalamu za rangi
gundi
pamba

https://youtu.be/d_2f097MsmU

Nini cha kufanya:



Paka rangi kurasa

Tenganisha pamba kwa kuvuta



Gundisha kwenye pamba

© 2023 truewaykids.com



© 2023 truewaykids.com

Kioo cha kuukuza Moyo

Utahitaji:

- Kiolezo kwenye kadi nyeupe
- Penseli za rangi/kalamu za rangi
- Gundi
- Mkasi
- Mfuniko mzuri wa plastiki

https://youtu.be/vN3O6mnWAf8

Nini cha kufanya:

1. Chapisha kwenye kadi nyeupe
2. Paka rangi katika picha
3. Muombe mtu mzima akate miwani ya kukuza na mioyo ya ndani
4. Weka plastiki ndani ya moyo na gundisha pande zote mbili kwa pamoja.

© 2023 truewaykids.com

© 2023 truewaykids.com



© 2023 truewaykids.com

© 2023 truewaykids.com

Muda wa kuabudu

Agiza kuimba wimbo wa kuabudu. Siyo ulioandaliwa na Trueway Kids.
Video za Yutube zitumike kwa matumizi binafsi tu.

The lord looks at heart

https://youtu.be/OzsoOy7YMWY

Man Looks On The Outside

https://youtu.be/yoQwSChEhtU

Looking At My Heart

https://youtu.be/AS0Dgv-iJPo

Muda wa maombi

Mshukuru Mungu kwa zawadi alizokupa.

Mwombe Mungu akusaidie kuwaona watu jinsi yeye anavyowaona watu.

Omba Mungu akusaidie umfanyie kila kitu Yeye.

Juma lijalo

Daudi na Goliathi

Kama bado hujafanya hayo, jiunge kwa barua pepe ili kupokea somo la wakati ujao.
truewaykids.com/subscribe/

© 2023 truewaykids.com